# Elimu ya Uwezekano wa Juu na Vipawa katika shule za umma za NSW – mwongozo kwa wazazi na walezi

Eimu ya Uwezekano wa Juu na Vipawa (High Potential and Gifted Education (HPGE)) husaidia wanafunzi wote wa shule za umma za NSW kuendelea kuwa na shauku na kukabiliana changamoto katika kujifunza kwao kukidhi mahitaji yao mahususi ya kujifunza. Inazingatia kwenye nyanja 4 (aina) za kuwezekana: ya kubuni, ya kiakili, ya kimwili na ya kijiamii kihisia.

## Nyanja 4 za uwezekano

Nyanja za uwezekano ni aina kuu 4 za uwezo wa asili ambao watu wanaweza kuwa nao. Mara nyingi huingiliana na huathiriana sana. Hizi ni nyanja:

**Nyanja ya ubunifu** – hurejea kwa uwezo ambao unatumia ubunifu, akili za kubuni na kufikia mawazo mapya. Uwezo huu unaweza kuonekana katika watoto kupitia jinsi wanavyoandika hadithi fupi, kutunga wimbo, kuchora bando, kutengeneza suluhu la kipekee kwa tatizo la hisibati, au kupanga ngoma.

**Nyanja ya akili** – hurejea kwa uwezo wa kuelewa mawazo magumu, kutatua matatizo, na kutimiza ujuzi. Kwa mfano, mtoto anaweza kujifunza kwa haraka na kwa rahisi, au kuonyesha ufahamu wa kina wa falsafa, sayansi au vitabu.

**Nyanja ya kimiwili** – hurejea kwa uwezo wa asili katika harakati za binadamu. Kwa mfano, wakati wa shughuli za michezo, za kushona, useremala au uhandisi. Uwezo huu unaweza kutambuliwa kwenye darasani na kiwanja cha kucheza, pamoja na kupitia fursa na mashindano ya shule za ziada ya mitaala na za jumuyia.

**Nyanja ya kijamii na kihisia** – hurejea kwa uwezo wa kudhibiti hisia zao na uhusiano na wengine. Uwezo huu unaweza kuonyeshwa kupitia mwingiliano na wanafunzi wenzao, walimu, na wazazi au walezi. Kwa mfano, mtoto anaweza kujiamini sana na mzuri katika kuongoza na kufanya kazi na wengine, au kuonyesha ustadi wa ujasiriamali.

## Jinsi shule zinavyosaidia wanafunzi wenye uwezo wa juu na vipawa

Uwezo wa mtoto unaweza kutofautiana, kwa hiyo anaweza kuhitaji aina mbalimbali za usaidizi na mafundisho. Kwa mfano:

**Wanafunzi wenye uwezo wa juu** ni wale ambao wana uzezo wa juu zaidi kuliko wanafunzi wa umri sawa, na wanaweza kufaidika kupewa changamoto zaidi.

**Wanafunzi wa vipawa** wana uwezo wa juu sana kulingana na wanafunzi wa umri sawa na wanaweza kukuza vipawa vyao kwa haraka na rahisi wanapopewa fursa.

**Wanafunzi wenye vipawa vya juu** wana uwezo wa kipekee na wanaweza kuhitaji marekebisho makubwa ili kukidhi mahitaji yao ya juu ya kujifunza.

Shule husaidia wanafunzi wenye uwezo wa juu na vipawa kupitia mbinu na mipango mbalimbali ya kufundisha. Hiyo inaweza kujumuisha:

- masomo ambayo yanawapa changamoto na kuwatia moyo wanafunzi
- shughuli za uboreshaji na programu za ziada za mitaala
- kuweka wanafunzi katika vikundi pamoja na wengine wenye uwezo sawa
- njia za juu za kujifunza kama vile kuongeza kasi (kupitia mtaala haraka zaidi) wakati zinapofaa
- usaidizi kwa kukuza ustawi na ustadi wa kijamii.

Lengo ni kuwasaidia wanafunzi huhama kutoka uwezekano wa juu hadi ufaulu wa juu kama ni sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati, lugha, sanaa, mchezo, uongozi au eneo lingine.

## Kila mwanafunzi ni pekee

Wanafunzi wenye uwezo wa juu wanaweza kutoka asili zozote, ikiwemo wale wenye ulemavu au kutoka asili mbalimbali na vikundi vya lugha. Wengine hufaulu vizuri sana shuleni tayari, wakati wengine wanaweza kuhitaji usaidizi ziada ili kufanya bora kwao. Ni kosa la uelewa wa kawaida kuwa wanafunzi wenye vipawa hawahitaji usaidizi kwani wengine wao wanahitaji usaidizi mahususi ili kuendelea kupenda mambo na kufanya vyema shuleni.

## Nini cha kufanya ikiwa unaamini kuwa mtoto wako ana uwezekano wa juu au anaweza kuwa mwenye vipawa

Ikiwa unafikiri mtoto wako anaweza kuwa na uwezo wa juu, tafadhali jadiliana huu pamoja na mwalimu wa mtoto wako. Wakati unapozungumza na mwalimu, tafadhali toa mifano ya mtoto anayofanya ambao inaweza kuwa ishara za uwezo wa juu au vipawa katika nyanja zile zozote.

Wazazi na walezi wana jukumu muhimu kwa kuhusika katika kujifunza kwa mtoto wao, kushiriki maarifa kuhusu mtoto wao na kufanya kazi kwa ushirikiano na shule.

## Sera ya HPGE

Sera ya Elimu ya Uwezekano wa Juu na Vipawa hutumia kwenye kila shule ya umma kote NSW. Inawasaidia walimu kutathmini na kutambua kile wanafunzi wenye uwezo wa juu na vipawa wanachohitaji na jinsi ya kuwapa fursa za kukua na kufanikiwa.

## Ni wapi pa kupata taarifa zaidi

- Kila shule ya umma katika NSW inatoa shughuli za HPGE. Tafadhali rejea kwenye tovuti ya shule ya mtoto wako ili kupata maelezo zaidi.
- Huenda kutaka kuzungumza na walimu wa mtoto wako kuuliza jinsi shule inavyosaidia wanafunzi wenye uwezo wa juu na wenye vipawa.
- Tembelea kwenye tovuti ya Elimu ya Uwezekano wa Juu na yenye Vipawa ya Idara ili kugundua sera hii na rasilimali.

## Huduma ya mkalimani wa simu

Iwapo unahitaji usaidizi wa mkalimani kuzungumza na shule ya mtoto wako kuhusu elimu ya uwezo wa juu na yenye vipawa, tafadhali piga simu kwa 131 450, umwambie mpokeaji lugha gani unachohitaji na umwombe apige simu shuleni.

Mpokeaji simu atakupa mkalimani kwenye simu kukusaidia na mazungumzo yako. Hutatozwa gharama kwa huduma hii.